

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**612**


**URAIA**

**Muda: Saa 3**

**Mwaka: 2022**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma maelekezo **yote** katika kijitabu chako cha kujibia.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha **mtihani**.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Mahakama Kuu ya Tanzania ina majukumu gani kwa wananchi? Ainisha majukumu manne.
2. Fafanua kwa ufupi kazi nne za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama kiunganishi cha serikali na wananchi.
3. Kwa kutoa mifano, tumia hoja nne kutofautisha kati ya jinsi na jinsia.
4. (a) Kiongozi mwadilifu katika muktadha wa somo la uraia ni kiongozi wa namna gani?  
(b) Mbinu gani zinaweza kutumika kurekebisha maadili mabaya katika jamii? Ainisha mbinu tatu.
5. Uchumi wa Taifa letu unategemea vyanzo gani vya mapato? Orodhesha vyanzo vinne.
6. Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) hufanya kazi kwa kutegemeana. Bainisha misingi minne inayoweza kutegemeana kwa nchi wanachama.
7. Bainisha athari hasi nne za Tanzania kujiunga katika Jumuiya za Kimataifa.
8. Machapisho bora ya ziada ya kufundishia somo la Uraia yana sifa gani? Bainisha sifa nne.
9. Kwa kutumia hoja nne, thibitisha kuwa azimio la kazi linahusiana na andalio la somo katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
10. Kwa kutoa mifano, eleza kwa ufupi malighafi nne zinazotumika kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia kwa wanafunzi wa Darasa la Sita.

## SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

11. Mwalimu Yona ni mahiri wa kuandaa andalio la somo na azimio la kazi la somo la Uraia. Eleza mambo matano anayozingatia mwalimu Yona wakati wa kufanya maandalizi hayo.
12. Tafiti zinaonesha kuwa, wanafunzi wenye ufaulu mzuri wanatoka katika familia zenye misingi bora ya maadili mema. Fafanua misingi sita inayoweza kutumika kujenga familia za wanafunzi wenye ufaulu huo.

13. Kwa kutoa mfano wa swali moja kwa kila ngazi, chambua ngazi sita za nyanja ya utambuzi kama zinazovyotumika katika mchakato wa upimaji wa wanafunzi.
  
14. Upo katika mafunzo kwa vitendo, mwalimu mkuu amekutaka kuwafundisha wanafunzi wa Darasa la Sita mada ndogo ya “Sera na Mipango ya Uchumi” kwa dakika 40. Kwa kuzingatia muundo wa andalio la somo la Uraia, andaa hatua za somo kwa kuzingatia vitendo vya ufundishaji, ujifunzaji na upimaji.